BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 11 Juni, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

151. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Pamoja na juhudi za Serikali na vyombo vyake katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji, imeonekana kuna baadhi ya viongozi wa Serikali wanaingilia kesi za ubakaji na kuwakingia kifua watuhumiwa. Mnamo tarehe 15/3/2018 Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi imepokea malalamiko Pemba kuwa baadhi ya wakubwa Serikali wanaingilia kazi za Jeshi la Polisi wanapowachukulia hatua wahalifu wa udhalilshaji.

(a) Je, Serikali inatambuwa viongozi wa ngazi mbali mbali ambao wanatumia nafasi zao kuingilia kesi za udhalilishaji kwa kuwakingia kifua watuhumiwa wasichukuliwe hatua.

(b) Kwa vile ipo Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma, hatua gani zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya kiongozi yeyote ambaye anatumia nafasi yake ya uongozi kuingilia kazi ya Polisi wanaposhughulikia watuhumiwa wa ubakaji na makosa mengine.

(c) Kwanini Serikali haiwachukulii hatua viongozi wenye tabia hizo ambao wanaifedhehesha Serikali ambayo imejifunga mkaja kupambana na vitendo vya udhalilishaji na ubakaji kwa nguvu zote.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ:

139. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika soko la matunda la Mombasa kumeonekana hali ya uchafu na jaa karibu na mahala wanapouza bidhaa za chakula kama matunda na jaa hilo linakera watu. Hali hii ni hatari kwa afya za watumiaji bidhaa zinazouzwa sokoni hapo.

(a) Je, hatua gani za haraka zinachukuliwa kuliondowa jaa hilo.

(b) Kuna mpango gani endelevu wa kuimarisha usafi wa masoko.

Wizara ya Fedha na Mipango:

159. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Serikali hufanya makisio na kupanga bajeti ili kupata mipango ya kutoa huduma kwa wananchi na Serikali yao lakini pamoja na kupanga huko, hutokea baadhi ya sekta kutotimiza malengo na kufanya bajeti kushindwa kutimia bila sababu maalum.

(a) Je, imeshawahi kutokea baadhi ya sekta kutotimiza malengo hayo ya bajeti bila sababu.

(b) Je, Serikali huchukua hatua gani kwa uongozi huo.

(c) Je, hatuoni watu kama hao wakiendelea kushindwa kukusanya kodi ni kuturudisha nyuma kimaendeleo.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

168. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa mwaka 2017, Idara ya Habari Maelezo ilitoa vibali kadhaa kwa ajili ya kupiga picha na uchukuaji habari katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar. Miongoni mwa Kampuni hizo zipo Kampuni za Kigeni.

(a) Je, katika kampuni ambazo zimepewa vibali vya kupiga picha na uchukuaji filamu, ni Kampuni ngapi za kigeni zilizopewa kibali.

(b) Je, Zanzibar hufaidika vipi kutoka kwa Kampuni zilizopewa vibali zinapofanya kazi ya kupiga picha na kuchukua filamu.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

234. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Wananchi wa Shehia za Mfenesini, Kama, Chuini na Kihinani katika Jimbo la Mfenesini wanakabiliwa na tatizo kubwa la maji safi na salama kwa kipindi kirefu hivyo kuleta shida kubwa kwao. Tatizo hilo kwa kiwango kikubwa linasababishwa na kupasuka kwa muda mrefu mabomba ya maji katika Shehia za Kama na Chuini pamoja na ubovu wa tangi la maji Kama. Na kwa kuwa viongozi wa Jimbo la Mfenesini wameshafanya juhudi kubwa za kuziarifu Mamlaka husika juu ya matatizo hayo.

(a) Je, ni Taasisi ipi inayotakiwa kurekebisha tatizo hilo ili wananchi wapate huduma hiyo ya maji.

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha matatizo hayo kutokutatuliwa zaidi ya mwaka mmoja.

Wizara ya Afya:

73. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kumekuwa na kilio kikubwa cha upungufu wa madaktari Kisiwani Pemba katika Hospitali na vituo vya afya.

(a) Kuna hatua gani za dharura zinachukuliwa kukabiliana na upungufu huo.

(b) Wapo Madaktari wameshaajiriwa Kisiwani Pemba lakini uajiri wao ukafutwa bila sababu za msingi, Serikali inasemaje kuhusu madai hayo.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

164. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Kuna watu walifanya kazi kama kuimba au kutunga nyimbo lakini watu hao wengine wameshafariki au ni wagonjwa na kazi hizo walizozifanya kuna watu wanazitumia na kupata fedha lakini hao waliofanya kazi hawapati malipo yoyote.

(a) Je, Wizara wanalijua hilo.

(b) Je, Wizara imechukua hatua gani ili kuhakikisha watu hao wanapata haki zao.

(c) Je, ipo Sheria ya kudai haki zao za sanaa hapa Zanzibar.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kwa mwaka 2018/2019.

Zanzibar,
11 Juni, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.